**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**

**Tovuti: www.hlpc.go.tz**

# TANGAZO

## MAOMBI YA MTIHANI WA USAJILI WA MWEZI APRILI 2025

Ofisi ya Msajili Baraza la Wataalam wa Maabara inawataarifu wahitimu wote wa kada ya maabara ya afya kuwa dirisha la maombi ya mtihani ya usajili litafunguliwa tarehe 04.02.2025 saa 03:00 asubuhi na kufungwa tarehe 15.03.2025 saa 9:30 alasiri.
Maombi yatafanyika kwa kwa kupitia mfumo wa HPRS hivyo waombaji wote watumie akaunti zao waliozotumia kufanya maombi ya usajili wa awali (PRP). Ili maombi ya mtihani yawe yamekamili lazima mwombaji awe amepata namba ya malipo (control number) kupitia akaunti yake ya mfumo wa HPRS. Malipo yafanyike kabla ya tarehe 15.03.2025 Saa 09:30 alasiri

Aidha, mhitimu ambaye alipata usajili wa awali kabla ya mfumo (Kabla ya Oktoba 2021) anatakiwa kutuma taarifa zifuatazo kupitia ujumbe mfupi wa maandishi kwenda namba 0734005777

- Majina kamili
- Barua pepe (email)
- Ngazi ya elimu ya kitaaluma
- Namba ya usajili wa awali (PRP)
- Namba ya simu

Taarifa hizo ni kwa ajili ya kutengezewa akaunti ya kumwezesha kufanya maombi ya mtihani. zoezi la kupokea taarifa hizo tarehe 02.03.2025 saa 09:30 alasiri.

Waombaji wote wanasisitizwa kufanya maombi ya mtihani kwa wakati ili kuepuka usumbufu

Ofisi ya Msajili inawatakia utekelezaji mwema

Imetolewa na:

Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara.
03.02.2025

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
03 FEB 2025
P.O.Box 743
DODOMA